TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# COSTECH Jarida

ISSN : 1827-7702 | TOLEO LA : 4 | SEPTEMBA, 2022

# COSTECH tunawafikia wabunifu wote nchi nzima - Dkt. Amos Nungu



Watumishi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) wakiwa na Mbunifu wa gari linalofanya kazi zaidi ya moja Bw. Elikana Mjungu Paulo (kushoto) mara baada ya kumtembelea Wilayani Ukerewe na kujua mahitaji yake.

*Ukurasa 10*



## Uzinduzi wa mkaa mbadala (RAFIKI BRIQUETTE)

*Ukurasa 11*

## COSTECH yasajili miradi ya utafiti 101

*Ukurasa 9*



*Jarida la COSTECH limechapwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Barabara ya Ali Hassan Mwinyi Road, Kijitonyama (Sayansi), Jengo la COSTECH, Dar es salaam, Tanzania | Simu: +255 22 2771358 au +255 22 277 4023 | Barua Pepe: dg@costech.or.tz | Tovuti: www.costech.or.tz*

## Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



Dkt. Amos Nungu
Mkurugenzi Mkuu - COSTECH

Kwa niaba ya Menejimenti na Wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), napenda kukukaribisha katika Jarida letu la mwezi toleo la mwezi wa Septemba 2022. Jarida hili linaelezea shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na COSTECH katika mwezi husika.

Kwa mwezi huu wa Septemba 2022, baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na COSTECH ni pamoja na kuendesha mafunzo ya kujengeana uelewa wa maswala ya Bioteknolojia kwa makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kusajili na kutoa vibali vya tafiti 101 zitakazofanyika hapa nchini. Shughuli nyingine ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya utafiti na ubunifu inayotekelezwa kwa ufadhili wa COSTECH hapa nchini, Kutoa mafunzo kwa wabunifu na watafiti namna ya kuendeleza kazi zao za ubunifu na utafiti hapa nchini.

Hizo ni baadhi kazi zilizotekelezwa katika mwezi wa Septemba, 2022. Nichukuwe fursa hii kukukaribisha kusoma taarifa mbali mbali kwenye jarida hili na kuomba maoni yako ya namna ya kuboresha jarida hili
Karibu sana.


## Bodi ya Wahariri

**Mwenyekiti**
Samson John Mwela

**Mratibu**
Dkt. Wilbert Bunini Manyilizu

**Mhariri Mkuu**
Bi. Mary Msungu Kigosi

**Mhariri**
Bw.Faisal Abdul Jalil

**Wajumbe**
Bi. Adeline Ajuaye
Bw. Mboyi Wishega
Bw. Emmanuel Girimwa
Bi. Bestina Daniel

**Msanifu**
Gabriel Chowo





Jarida la COSTECH limechapwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi Road, Kijitonyama (Sayansi), Jengo la COSTECH, Dar es salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2771358 au +255 22 277 4023
Barua Pepe: dg@costech.or.tz
Tovuti: www.costech.or.tz

# TAARIFA YA AWALI YA MAENDELEO YA UCHAMBUZI WA SERA YA ELIMU YAPOKELEWA - ZANZIBAR

**Dodoma | Sept 12, 2022**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe Prof Adolf Mkenda pamoja na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Mhe Lela Mohamed tarehe 12 Septemba 2022 wameshiriki kikao kazi cha kamati ya mapitio ya sera ya elimu.

Katika kikao kazi hicho, Mawaziri hao wamepokea taarifa ya awali ya maendeleo ya kazi ya uchambuzi wa sera ya elimu.

Timu hiyo inayofanya kazi Jijini Dar es salam inaendelea na uchambuzi wa Sera ya Elimu ya mwaka 2014 ambapo Sera hiyo ilifuta sera ya elimu ya mwaka 1995.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapitia sera hiyo ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili mwaka 2021 jijini Dodoma



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda wakati wa kikao cha kupokea taarifa ya awali ya maendeleo ya uchambuzi wa Sera ya Elimu*



*Washiriki wa kikao kazi cha mapitio ya awali ya maendeleo ya uchambuzi wa Sera ya Elimu.*

# Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wajengewa uelewa wa bioteknolojia ya kisasa

**Zanzibar | Sept 24, 2022**



*Picha ya pamoja ya viongozi mbalimbali mara baada ya mafunzo ya kujengewa uelewa wa Bioteknolojia ya kisasa katika mkutano wa siku 1 uliofanyika tarehe 24 Septemba, 2022 katika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) – Zanzibar.*

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kupitia Kurugenzi ya Uratibu na Uendelezaji tafiti (DRCP) kwa kushirikiana na Tume ya Mipango-Zanzibar iliratibu mkutano wa siku 1 tarehe 24 Septemba 2022, katika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuwajengea uelewa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya Bioteknolojia ya kisasa na usimamizi wake.

Mkutano huo ulihudhuriwa na ujumbe wa washiriki 77 na kuongozwa na Mwenyekiti ambae ni Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar , Mhandisi Zena Mohamed Saidi, Makatibu na Manaibu Wakuu 14 toka Wizara tofauti, Wakurugenzi toka Idara mbalimbali za Serikali, Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Juu, Taasisi za Utafiti na Mamlaka mahiri, Wawakilishi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Sekretarieti ya Makatibu Wakuu, pamoja na waratibu wa mkutano huo wawakilishi kutoka COSTECH na Tume ya mipango ya Zanzibar.

Mkutano huo pia ulilenga kupokea mapendekezo ya kuboresha rasimu ya Mfumo wa Usimamizi wa Bioteknolojia ya kisasa visiwani Zanzibar na kukuza uelewa wa pamoja juu ya masuala ya bioteknolojia ya kisasa na uthibiti wake kwa watoa maamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumzia Uandaaji wa Mfumo wa usimamizi wa bioteknolojia, Zanzibar, Kamishna wa Utafiti, Tume ya Mipango. Dkt. Afua Mohamed alisisitiza kuwa COSTECH imekuwa ikiendeleza kazi hii kwa miaka sita (6) mfululizo hadi sasa na kuwezesha kuwepo na rasimu inayopendekeza Mfumo wa Kitaifa wa Uthibiti wa Biotenolojia ya kisasa utakaojulikana kama Zanzibar Biosafety framework (ZBF).

Aidha, kazi za uandaaji wa mfumo huo (ZBF) zimefanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar (MANRLF), Idara ya Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Tume ya Mipango-Zanzibar.

“Mfumo huu unategemewa kutumiwa na wadhibiti, watengenezaji wa bioteknolojia, watunga sera na wadau wengine wenye dhamana ya kuhakikisha matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa ikiwa ni pamoja na bidhaa zilizotengenezwa kutokana na Viumbe Vilivyobadilishwa Jeni (GMOs) Zanzibar” alisema Dkt. Afua.

Mkutano huo ulihitimishwa kwa washiriki kuja na azimio lilopendekeza kuwa Rasimu ya Mfumo wa Usimamizi wa Bioteknolojia ya kisasa pamoja na kanuni zake za usimamizi uwasilishwe kwenye Baraza la Mapinduzi Zanzibar kabla ya mwezi Disemba mwaka 2022.



*Sehemu ya washiriki wa Makatibu Na Naibu Makatibu Wakuu Wa Serikali Ya Mapinduzi Ya Zanzibar wakichangia mada katika mkutano wa siku 1 tarehe 24 Septemba 2022 wa Bioteknolojia Ya Kisasa, katika ukumbi wa Benki ya Tanzania (BOT).*

# Wafanyakazi wa COSTECH wapata mafunzo ya Stress Management

**Dar es salaam | Sept 22, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeendesha mafunzo ya afya ya Usimamizi wa Msongo wa Mawazo (Stress Management) ikilenga kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wake.
Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 22 Septemba 2022 katika ukumbi mkubwa wa mikutano uliopo ndani ya Jengo la Ofisi za COSTECH - Sayansi (Kijitonyama) - Jijini Dar es salaam.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Ndg. Immanuel I Mgonja alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kuongeza tija na ufanisi wa utedaji kazi wa kila siku kwa watumishi wa Tume ili kuhakikisha inafikia malengo iliyojiwekea na kuhakikisha utekelezaji wa Mpango-Mkakati wa Taasisi wa miaka 2021/2022 mpaka 2025/2026.

Mafunzo hayo yameendeshwa na Mkufunzi kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dkt. Garvin Kweka aliewasilisha mada mbalimbali na kusisitiza kuzingatia muda wa ufanyaji kazi ambapo ni muhimu ili kusaidia kuondoa changamoto ya kufanya kazi mpaka masaa yasiyo ya kazi kwani huathiri ufanisi wa utendaji kazi.



*Wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia COSTECH wakifuatilia semina ya Stress Management iliotolewa na Dkt. Garvin Kweka kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.*




# COSTECH kushirikiana na NOTAP kuendeleza teknolojia

**Nigeria | Sept 08, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeahidi kuendeleza mashirikiano na Shirika la NOTAP la nchini Nigeria kwa lengo la kutangaza Teknolojia za nchi hizo mbili kupitia ujumbe wa Tanzania uliotembelea kuanzia tarehe 7 hadi 8 Septemba 2022 chini ya uratibu wa Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchini Nigeria

Akizungumza katika mkutano huo, Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Mhe. Dkt Benson Bana alishukuru Shirika la NOTAP kwa kukubali kuendelea kuhuisha uhusiano ulioanzishwa kwa kipindi cha miaka kumi toka mwaka 2012 mpaka sasa.

"Tunahitaji kuimarisha ushirikano kati ya nchi hizi mbili katika masuala yenye kuleta tija na manufaa kwa pande mbili kama Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU). Ushirikiano miongoni mwa nchi za kiafrika ulioasisiwa na mababu zetu wakati wa vita vya mapambano dhidi ya ukoloni na sasa ushirikiano huo ni katika masuala ya Teknolojia" alisema Mhe. Dkt Bana.

Dkt. Bana anafafanua kuwa mwezi Juni mwaka 2021 alitembelea Shirika la NOTAP na kujulishwa kuwa COSTECH na NOTAP wameanzisha mahusiano toka mwaka 2012 katika nyanja ya Uhawilishaji wa Teknolojia na niliandikia barua COSTECH ya kushauri kuhuisha mahusianao hayo ambapo Taasisi hizo ziliwasiliana kwa njia ya mtandao tarehe 20 Januari 2022 na kupata mwaliko kutembelea NOTAP huko Abuja kwa mazungumzo zaidi. Akizungumza katika mkutano huo, Dkt. Amos Nungu alimshukuru Balozi wa Tanzania Dkt. Bana kwa jitihada kubwa alizofanya kuhuisha mahusiano baina ya COSTECH na NOTAP.

"Tunahitaji kujifunza kutokana na uzoefu wa Nigeria katika kuunganisha viwanda na taasisi za utafiti na maendeleo. Tunaahidi kutoa ushirikiano kamili katika kutekeleza yale tutakayokubaliana pia natarajia kuona maofisa wa NOTAP wakitembelea COSTECH" alisema Dkt. Nungu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NOTAP Dkt DanAzumi Ibrahimu alimshukuru Balozi wa Tanzania kwa jitihada zake zilizopelekea kuhuishwa kwa mahusiano hayo kati ya COSTECH na NOTAP.

"Nigeria na Tanzania zinachangamoto zinazofanana na njozi moja katika kupambana ili kupata uhuru wa kiteknolojia. Hivyo ina tija kwa nchi hizi mbili kufanya kazi Pamoja kwa kusaidiana" alisema Dkt Ibrahim.



*Picha: Mkurugenzi mkuu NOTAP Dkt DanAzumi Ibrahim wa kwanza kushoto akisalimiana na mkurugenzi mkuu COSTECH Dkt. Amos Nungu wa kwanza kulia, wa pili kulia ni Balozi wa Tanzania nchini Nigeria Mhe. Dkt. Benson Bana*



*Waziri wa Sayansi na Teknolojia wa Nigeria wa tatu kushoto Pamoja na mkurugenzi mkuu-COSTECH wa pili kushoto na mkurugenzi mkuu-NOTAP wanne kutoka kulia kwenye picha ya Pamoja.*



# COSTECH yapokea ujumbe wa programu ya FSBL kutoka nchini Uingereza

**Dar es salaam | Sept 06, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) tarehe 6 Septemba 2022 imepokea wageni kutoka Chuo Kikuu cha Fizikia cha nchini Uingereza kwa lengo la kutembelea mradi wa FSBL (Future STEM Business Leader) unaowajengea uwezo walimu na wanafunzi katika masomo ya Sayansi, Teknolokojia, Hisabati na Uhandisi nchini.

Akizungumza wakati akifungua kikao hicho, Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi (DCS) kutoka COSTECH,

Bw. Immanuel Mgonja alisema wanafunzi wengi wamekuwa hawavutiwi na masomo ya Sayansi ikiwemo somo la fizikia (Physics) kwasababu ya kuwepo kwa changamoto ya ufundishaji wa walimu kwa njia ya nadharia zaidi kuliko vitendo.

"kumekuwa na changamoto ya baadhi ya walimu kukosa ubunifu na mifano hai wakati wa ufundishaji, hivyo hupelekea Vijana wengi kutokuwa na mwamko wa kusoma masomo ya Sayansi ikiwemo fizikia ni kutokana na uchache wa walimu na vifaa vya kufundishia katika sekta ya elimu'' Bw. Mgonja aliongeza

Ujumbe huo unatarajia kuanzisha mpango wa miaka 5 wa ufadhili ambapo watatoa kiasi cha Euro Milioni 20 hadi Euro Milioni 25 sawa na Tsh. Bilioni 57 za Kitanzania.

Aidha mpango wa ushirikiano huo wa Afrika na nchi za Jumuiya ya Madola wa kifizikia kupitia programu AUPP (Africa - UK Physics partnership) utakaotembelea nchi tano (5) za Afrika ikiwemo Taifa la Tanzania, Kenya, Uganda, Afrika Kusini na Rwanda ili kuibua watafiti wachanga na wenye vipaji waweze kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi (hali ya hewa) na nishati mbadala.

Akifafanua zaidi kuhusu msimamizi wa mradi wa FSBL Tanzania, Meneja Uhusiano wa Kimataifa, Bi. Linsey Simkin amesema ni muhimu kuendeleza juhudi za kuchochea wanafunzi kupenda masomo ya STEM yanayosimamiwa na Atamizi ya DTBi iliyopo chini ya COSTECH.

Bi Linsey aliambatana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Kimataifa , Bw. Dominic Hurley Pamoja na Makamu Mkurugenzi Mtendaji (Deputy CEO) kutoka Idara ya Fizikia ya Uingereza.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Uratibu na Uendelezaji wa Tafiti (DRCP) COSTECH Dkt. Paul Ochang'a aliwakabidhi wajumbe Mwongozo wa Kitaifa wa Vipaumbele vya Utafiti na kuongeza kuwa COSTECH iliandaa mwongozo huo kupitia ukurasa wa 19 unazungumzia sekta hizo mbili ya nishati mbadala (Renewable Energy) na Mabadiliko ya tabia ili kutoa hamasa na nafasi kwa wadau wa Tume kushiriki katika kujenga uwezo wa watafiti wachanga, mashirikiano na miundombinu ya uendeshaji tafiti nchini.

Dkt. Paul amesema kumekuwa na uwoga kwa wanafunzi wa kike kuchukua masomo ya Sayansi jambo linalopelekea kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika ufundishaji wa somo husika.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Atamizi ya DTBi, Dkt Erasto Mlyuka, alisema Tume imeweka mazingira wezeshi kupitia Mfuko wa Taifa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) ambayo kazi yake ni kupokea fedha za wafadhili wa ndani na nje na kusimamia matumizi yake.

Kwa upande wake, Meneja Mradi wa FSBL inayoratibiwa COSTECH chini ya Atamizi ya DBTi, Bi. Josephine Sepeku alisema mafanikio yatokanayo na mradi huo kwasasa ni mzuri kwani ulianza na jumla ya shule sita (6) na sasa umefikia jumla ya shule 17 pamoja na kuongeza wigo na wabia wa mradi ambapo ulianzishwa Mkoani Dar es Salaam pekee na kwasasa umefikia Mkoa wa Arusha.



*Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi COSTECH Bw. Imanuel Mgonja, wageni kutoka Chuo cha Fizikia Uingereza na baadhi ya watumishi wa COSTECH wakati wa kupokea ujumbe wa mradi wa FSBL.*



*Picha ya pamoja  watumishi wa COSTECH Pamoja na ugeni kutoka Uingereza mara baada ya kikao.*

# COSTECH yasajili miradi ya utafiti 101



**Dar es salaam | Sept 28, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kupitia Kurugenzi ya Uratibu na Uendelezaji wa Tafiti (DRCP) imesajili vibali 101 vya utafiti kwa kipindi cha mwezi Septemba ili kusajili miradi ya kitafiti itakayoongeza tija na kufikia dhana ya maendeleo endelevu kwa haraka.

Akifafanua kuhusu twakimu hizo, Afisa Uratibu Tafiti Mkuu toka Kitengo cha Usajili wa Miradi ya Utafiti Dkt. Joseph Maziku amebainisha kuwa COSTECH imefanikiwa kuwasilisha vibali vya tafiti 101 ndani ya mwezi mmoja.

Dkt Maziku anafafanua kuwa miradi mipya iliyosajiliwa kupitia mfumo wa vibali ni 70 sawa na asilimia 69.3% , vibali 25 vimehuishwa kwa kuongeza muda wa matumizi (extension) sawa na asilimia 25% pamoja na vibali 6 vilivyohitaji marekebisho ni sawa na asilimia 6 ya vibali vyote vilivyotolewa kwa mwezi Septemba ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2022.

Aidha, mafanikio hayo yamepatikana kupitia idhini ya miradi 101 ilioidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya Uidhinishaji miradi kupitia Mkutano wake wa 184 uliofanyika tarehe 28 Septemba 2022 na kukidhi maeneo yote manne (4) ya mawanda mapana ikijumuisha Sayansi Jamii asilimia 35% , Sayansi ya Matibabu na Afya asilimia 18% , Sayansi ya Kilimo na Mifugo asilimia 13%, Sayansi Asilia asilimia 32% na kuhitimishwa na eneo la Uhandisi na teknolojia sawa na asilimia 2%.

Aidha, Dkt. Maziku ameongeza kuwa Kamati iliidhinisha jumla maombi mapya 36 bila masahihisho na vibali 29 vilirejeshwa na kuongezewa muda wa maboresho, maombi mapya matano (5) yalikataliwa na kamati kuidhinisha jumla ya maombi ya miradi 6 na mingine 25 ilirudishwa kwa maboresho zaidi

Katika kikaokazi hicho, Kamati iliidhinisha miradi mingi katika nyanja za Sayansi ya Jamii, Sayansi Asilia, Uhandisi na Teknolojia na hakukuwa na mradi hata mmoja wa mtafiti uliosajiliwa katika nyanja ya Binadamu na Sanaa.

Miradi ya utafiti iliyosajiliwa inatekelezwa katika mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara inayojumuisha Mkoa wa Dar es Salaam, Arusha, Manyara, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza, na Iringa.

Dkt Maziku anafafanua kuwa kati ya maombi 101 yaliyowasilishwa Kamati iliidhinisha maombi mapya 29 kwa maboresho na maombi mapya 5 yalikataliwa na wakaguzi na kuongeza kuwa jumla ya miradi 25 na mingine 6 ilipitishwa ikijumuisha vibali 82 vya utafiti vilitolewa kwa Watanzania.

Watafiti 38 sawa na asilimia 46% , Wageni Wakazi Watafiti 44 sawa na asilimia 54% huku Taifa la Marekani likiongoza kwa idadi kubwa ya kusajili miradi ikifuatiwa na Taifa la Tanzania na Uingereza kwa kipindi cha mwezi Septemba 2022

Akitamatisha maoni yake amesema COSTECH imelenga kusajili na kutoa vibali kwa angalau watafiti 600 kufikia Juni 2023. Idadi ya watafiti na miradi ya utafiti inatarajiwa kuongezeka kwa sababu ya kuondolewa kwa vizuizi vya kusafiri na nchi nyingi baada ya kupungua UVIKO 19.



# COSTECH tunawafikia wabunifu wote nchi nzima

**Dar es salaam | Sept 29, 2022**

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dkt. Amos Nungu akijibu maswali ya wasikilizaji katika mahojiano yaliyofanyika katika kituo cha Utangazaji cha CLOUDS MEDIA kupitia programu ya PowerBreakfast tarehe 29 Septemba 2022 - Mikocheni - Jijini Dar es Salaam

"COSTECH kwa niaba ya Serikali tunawafikia wabunifu wote nchi nzima, sasahivi tumeanza mkakati wa kuanzisha kumbi ya ubunifu kule Zanzibar kwasababu COSTECH ni Taasisi ya Kimuungano na tupo katika hatua za awali za kukamilisha mchakato huo" alisema Dkt Nungu

Dkt. Nungu alitoa ufafanuzi kuhusu umuhimu wa wabunifu wachanga kufuata taratibu zilizowekwa na Serikali kupitia Taasisi hiyo ya COSTECH chini ya Kurugenzi ya Kituo cha Uendelezaji na Uhawilishaji wa teknolojia (DCDTT) inayoratibu kumbi bunifu ya BUNI Hub pamoja na Atamizi ya DTBi zilizopo chini ya COSTECH.

Aidha, Dkt. Nungu alisema kwa upande wa mbunifu aliyebuni gari linalofanya kazi zaidi ya moja kutoka katika wilaya ya Ukerewe alifikiwa na Serikali kupitia COSTECH na aliweza kusaidiwa namna ya kufanya usajili ili hilo gari liweze kuingia barabarani na kufanya kazi. Dkt. Nungu alijibu swali kutoka msikilizaji aliyetaka kujua taarifa za mbunifu huyo.



*Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dkt. Amos Nungu akifanya mahojiano na Kipindi cha Powerbreakfast alipotembelea Studio hizo zilizopo Mikocheni – Jijini Dar es alaam.*

# Uzinduzi wa mkaa mbadala (RAFIKI BRIQUETTE)



**Dodoma | Sept 12, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) maarufu kama NFAST kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Uchimbaji Madini (STAMICO) imeratibu uzinduzi wa Nishati ya Mkaa mbadala unaofahamika kwa jina la "Rafiki briquette" utokanao na makaa ya mawe pamoja na taka ngumu.

Uzinduzi huo ulifanyika Siku ya maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Shirika la STAMICO yaliyofanyika jijini Dodoma tarehe 12 Septemba 2022 - Jijini Dodoma.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Meneja Usimamizi wa Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia - MTUSATE toka COSTECH, Bw. Ntufye Mwakigonja alisema kwamba COSTECH inajivunia kuwa sehemu ya mafanikio katika Maadhimisho ya Miaka 50 ya Shirika la STAMICO kwa kusaidia upatikanaji wa mkaa huo mbadala ambao ni salama, nafuu kwa watumiaji na rafiki wa mazingira.

Katika uzinduzi huo, COSTECH kupitia mfuko wa MTUSATE ilitoa ufadhili wa kiasi cha fedha cha Shilingi Milioni 43.2 kugharamia utafiti uliofanikisha uvumbuzi wa mkaa huo wenye ufanisi zaidi kulinganisha na nishati nyingine za mkaa zinazotumika kwa sasa.



*Mbunifu wa mkaa mbadala akielezea namna unavyotengenezwa siku ya uzinduzi huo wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la STAMICO jijini Dodoma.*

# COSTECH yapatiwa mafunzo ya maadili na KAMAA



**Dar es salaam | Sept 30, 2022**

*Mkurugenzi wa Uratibu na Uendelezaji Tafiti (aliesimama kushoto) akifungua Kikao cha Maadili na Nidhamu kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi , Bw. Immanuel I. Mgonja wakati wa ufunguzi wa Mafunzo ya Kamati ya Maadili na Nidhamu maarufu kama KAMAA mbele ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) hawapo pichani katika Ukumbi wa Roud uliopo COSTECH – Jijini Dar es salaam.*

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) tarehe 30 septemba 2022 imepokea ujumbe kutoka kamati ya Maadili na Nidhamu maarufu kama KAMAA kwa lengo la kuwajengea uwezo watumishi wa ndani wa COSTECH kufahamu taratibu za utendaji kazi.

Akimuwakilisha Mkurugenzi Mkuu wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Uratibu na Undelezaji Tafiti (DRCP) alisema ni muhimu kuzingatia yale yatakayofundishwa na wataalamu wa KAMAA.

Mafunzo hayo yalihitimishwa na Mkurugenzi wa Uratibu na Undelezaji Tafiti (DRCP), Dkt. Bugwesa Katale aliyekuwa ameambatana na Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi kutoka COSTECH, Bw. Immanuel I. Mgonja pamoja na watumishi wote kutoka Kurugenzi nne (4) na Vitengo vyote vinne (4) vilivyopo Chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).



*Sehemu ya Watumishi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) wakifuatilia mafunzo ya Kamati ya Maadili na Nidhamu maarufu kama KAMAA*



# Wabunifu wachanga wanolewa COSTECH

**Dar es salaam | Sept 9, 2022**

Ili kuhakikisha Serikali inafikia adhma yake ya kuendeleza na kukuza matumizi ya Sekta ya TEHAMA nchini Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeendesha zoezi la kunadi bunifu changa kwa vijana 42 wa kundi la Vyuo Vikuu nchini kupitia programu Buni Talent Pool inayoratibiwa na kumbi mama wa Buni iliyofanyika terehe 9 Septemba 2022 - Sayansi (Kijitonyama) Jijini Dar es salaam.

Programu hiyo ilihitimishwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH Bw. Imanuel I. Mgonja kwa zoezi la ugawaji vyeti kwa washiriki wote na kikundi walichoandaa KAZI FASTA waliibuka washindi.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mtaalamu wa Mahusiano Buni Hub, Bi. Promise Mwakale alisema programu hiyo ina miaka saba sasa (7) na imedumu kwa wiki kumi (10) mfululizo ikianza mwezi Julai mwaka huu mpaka Septemba 2022 ambapo ilichukua wanafunzi toka Vyuo Vikuu vinne (4) ikilenga kusaidia vijana wengi zaidi kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Bi. Mwakale anaongeza kuwa programu hii imewezesha vijana kuandaa bunifu zenye tija na kuziwasilisha kwa jamii ili kutathimini ufanisi wake na kuzibadilisha kutoka kifaa cha mfano ( prototypes ) kwenda kuwa huduma au bidhaa kamili.



*Bi Promise Mwakale akitoa maelezo wakati kufunga program ya Buni Talent Pool inayoandaliwa na ukumbi mama wa bunifu wa Buni Hub.*

"Leo tunamaliza programu ya Talent Pool ambayo vijana 42 wanahitimu, toka Julai hapa COSTECH tumepitia na kuangalia mawazo yao, kutengeneza timu, wakabadilishana mawazo kwa ajili ya kuyaweka vizuri," amesema Mwakale.

Aidha, Bi Mwakale amevitaja Vyuo Vikuu vishiriki ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM - CoICT), Taasisi ya Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Taasisi ya Uhasibu (TIA) na Chuo Kikuu Ardhi (ARU).

Kwa upande wake, mhitimu wa programu hiyo, Ibrahim Laseko, amesema mafunzo hayo yamewapa nafasi ya kujifunza kuandaa wazo kutokana na changamoto zinazoikabili jamii na kupitia kikundi chake wameanzisha mtandao unaofahamika kwa jina la KAZI FASTA, ambao huwakutanisha waajiri na waajiriwa wanaotafuta kazi.

"Tuliumba wazo, na kwa sasa ni Application tunayoifanyia kazi inaitwa Kazi Fasta, kwa sasa haijakamilika ila itakuwa App ndani ya muda mchache na tumelenga watumiaji watakuwa vijana ambao wenye uwezo wa kuingia kwenye mtandao kufanya kazi mbalimbali ili kujipatia kipato hii itasaidia kuondokana na watu kukaa vijiweni na kusubiria kazi ambazo hazipo," amesema Laseko, ambaye ni mhitimu wa Taasisi ya Uhasibu (TIA).

Naye, Teddy Mick toka Chuo Kikuu Ardhi (ARU), amesema Programu hiyo imewapa nafasi ya kujua jinsi gani wanaweza kuendeleza au kuanzisha biashara au kuandaa kitu kipya kwa ajili ya jamii: Tumejifunza jinsi gani tunaweza fanya biashara au kitu ninachotaka kuanzisha kwenye Sayansi na Teknolojia.

Teddy amefafanua katika kundi lake lililotokana na programu hiyo, wamefanikiwa kuanzisha mtandao 'Application' inayopatikana kupitia simu za kiganjani ili kuwakutanisha wagonjwa na madaktari.

namna watakavyoendeleza utafiti pamoja na vigoda ambavyo vinasaidia kuchochea maendeleo ya bunifu pamoja na tafiti zinazofanywa.



*Mmoja wa kijana aliyekuwa kwenye program ya Buni Talent Pool akionyesha ubunifu walioubuni katika kundi lao.*



*Mkurugenzi wa huduma za taasisi Bw. Imanuel Mgonja akimpa cheti mshiriki wa Buni Talent Pool.*

TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# COSTECH



# Hongera

## Dkt. Amos Nungu

Menejimenti na Wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) tunakupongeza Dkt. Amos Muhunda Nungu kwa kuteuliwa na Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein M. Bashe (MB) kuwa **Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).** Uteuzi huo ni wa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 24 Agosti 2022

# Matukio katika Picha

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dkt Amos Nungu ameendesha Mkutano na watumishi wa Tume hiyo kwa siku moja (1) tarehe 4 Oktoba 2022 katika ukumbi wa mikutano COSTECH kuzungumzia utendaji kazi wa Taasisi – Sayansi (Kijitonyama) Jijini Dar es salaam.



*Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dkt. Amos Nungu (kulia) pamoja na watumishi wengine wa COSTECH wakifuatilia wasilisho la NOTAP kutoka kwa Dkt. Gerald Kafuku (Pichani hayupo) katika mkutano uliofanyika tarehe 4 Oktoba 2022, katika ukumbi wa mikutano wa COSTECH.*



*Mkurgenzi wa Huduma za Taasisi, Bw. Imanuel I Mgonja (Mwenye koti la Kijivu), Meneja Usiamaizi Rasimali Watu, Bw. Mboyi Wishega (wakwaanza kulia) na Kaimu Mkurgenzi wa Atamizi ya DTBI, Dkt Earsto Mlyuka (wakwanza kushoto) na sehemu ya watumishi wa COSTECH wakifuatilia Mkutano wa Mkurugenzi Mkuu na Watumishi wa COSTECH uliofanyika kwa siku ya siku moja (1) tarehe 4 Oktoba 2022 uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa COSTECH uliopo Sayansi (Kijitonyama) Jijini Dar es salaam.*



*Afisa Uratibu Mtafiti, Bw. Festo Maro akitoa akiuliza swali wakati wa Mkutano wa Mkurugenzi Mkuu na Watumishi wa COSTECH uliofanyika kwa siku ya siku moja (1) tarehe 4 Oktoba 2022 uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa COSTECH uliopo Sayansi (Kijitonyama) Jijini Dar es salaam..*



*Sehemu ya watumishi wa COSTECH wakifuatilia Mkutano wa Mkurugenzi Mkuu na Watumishi wa COSTECH uliofanyika kwa siku ya siku moja (1) tarehe 4 Oktoba 2022 uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa COSTECH uliopo Sayansi (Kijitonyama) Jijini Dar es salaam..*